

MFALME MTUKUFU

Zab. 24 : 1-6 (K) 7, 10

Prudence Rweyongeza
16.12.2019
Dodoma

Wimbo wa katikati
Jumapili ya 4 Majilio, Mwaka A

1. Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana/ dunia na wote wakaao ndani yake;
Maana ameiweka misingi yake juu ya bahari/ Na juu ya mito ya maji aliithibitisha.
2. Ni nani atakayepanda katika mlima wa Bwana/ Ni nani atakayesimama katika patakatifu pake;
Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe/ asiyeinua nafsi yake kwa ubatili.
3. Atapokea baraka kwa Bwana/ Na haki kwa Mungu wa wokovu wake;
Hiki ndicho kizazi cha wamtafutao/ Wakutafutao uso wako, Ee Mungu wa Yakobo